# صَلَاةُ العِيْدِ

## سُنَنُهُ وَآدَابُهُ

# SWALA YA EID

## Sunnah zake na Adabu zake

Mwandishi
Abu Halima Arafat bin Mahmoud

**Ni ipi hukumu yake:** Kuna khilafu baina ya Maulamaa kuhusu hukumu ya swala ya Eid, lakini kauli iliyo na nguvu ni kwamba hukumu yake ni wajibu, kwa sababu Mtume -Swala na Salamu zimshukie- aliwaamrisha mpaka wanawake wenye hedhi kuhudhuria katika viwanja vya kuswalia Eid, kwa hadithi ya Ummu 'Atwiyya -Allaah amridhie-:

**«أَمَرَنَا - تَعْنِي النَّبِيَّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ - أَنْ نُخْرِجَ فِي الْعِيدَيْنِ، الْعَوَاتِقَ، وَذَوَاتِ الْخُدُورِ، وَأَمَرَ الْحُيَّضَ أَنْ يَعْتَزِلْنَ مُصَلَّى الْمُسْلِمِينَ»**

**"Alituamrisha -Mtume Swala na Salamu zimshukie- kuwatoa wanawake baleghe (vigori) na wanawake bikra (waliostiriwa majumbani), kwenda kuhudhuria swala za Eid mbili, na akawaamrisha wanawake wenye hedhi kujitenga na mahala pa kuswali waislamu (wakae nyuma ya watu)"**[1].

### 1. Kuoga na kujipamba kwa ajili ya 'Idd:

Imepokewa kutoka kwa baadhi ya Maswahaba akiwemo Ibn Umar -Allaah amridhie-, kwamba alikuwa anaoga siku ya Eid kabla ya kwenda kuswali na pia hapana vibaya kuoga kabla au baada ya swala ya alfajri.

Amesema Imam An Nawawi -Allaah amrehemu-: **"Amesema Imam Shafi' na maulamaa wakubwa wa fiqhi (katika madhehebu ya Kishafi), kwamba inapendekezwa kuoga kwa ajili ya swala ya Eid mbili, na hakuna khilafu yoyoote katika jambo hili, na mategemeo yake ni athari ya Ibn Omar na kupigia kiasi siku ya Ijumaa.**

---

[1]- Bukhari (980) na Muslim (890).

**Ama kuhusu wakati sahihi wa kuoga kuna kauli mbili zenye nguvu, (moja inasema): Baada ya swala ya asubuhi, ameliweka wazi hilo (Imam Shafi') katika kitabu cha Al-Ummu, na kauli iliyo sahihi zaidi katika hizo mbili, na ndio makubaliano ya maulamaa wakubwa (wa madhehebu ya Kishafi) ni kwamba inajuzu baada ya swala ya asubuhi na kabla yake"**[2]**.**

## 2. Sunna ni kula tende kabla ya kwenda kuswali Eid al-Fitr

Kutoka kwa Anas -Allaah amridhie- amesema:

**«كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لاَ يَغْدُويَوْمَ الفِطْرِحَتَّى يَأْكُل تَمَرَاتٍ» قَالَ: «وَيَأْكُلُهُنَّ وِتْرًا»**

**"Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alikuwa harauki siku ya Eid al-Fitr mpaka ale tende chache".** Amesema: **"Akila kwa idadi ya witri"** [3]**.**

Ama swala ya Eidi al-Adh'ha kwa hadithi ya Buraida kutoka kwababa yake -Allaah amridhie- amesema:

**«كَانَ النَّبِيُّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ لاَ يَخْرُجُ يَوْمَ الفِطْرِحَتَّى يَطْعَمَ، وَلاَ يَطْعَمُ يَوْمَ الأَضْحَى حَتَّى يُصَلِّيَ»**

**"Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alikuwa haendi kuswali siku ya Eid al-Fitr mpaka ale, na siku ya Eid al-Adh'ha hali kitu mpaka amalize kuswali"**[4]**.**

Amesema Ibn Hajar -Allaah amrehemu-: **"Amesema Al-Muhallab: Hekima ya kula kabla ya kuswali ili asije akadhani mwenye kudhani kwamba ni lazima (kwake) kujizuia na kula mpaka baada ya swala ya Eid, kana kwamba (Mtume) alikusudia kuifunga dhana hiyo. Na wengine wamesema: Wakati ilipokuja ruhusa ya kula baada tu ya kumaliza ibada ya funga, ikapendekezwa kufanya haraka kula kwa ajili ya kutekeleza**

---

[2]- Al-Majmuu' (Jz. 5, Uk. 7).
[3]- Bukhari (953).
[4]- Sunan Tirmidh (542).

**amri ya Allaah Ta'alaa. Ama hekima ya kuchelewesha kula siku ya Eid al-Adh'ha ni kwa sababu siku hiyo imewekwa sheria ya kuchinja mnyama na kula sehemu katika mnyama huyo, kwa hiyo ikapendekezwa kuwa kifungua kinywa chake ni kula sehemu ya nyama hiyo"**[5]**.**

## 3. Sunna ni kuswali swala ya Eid kiwanjani:

Kutoka kwa Abu Said -Allaah amridhie- amesema:

«كَانَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ يَخْرُجُ يَوْمَ الفِطْرِ وَالأَضْحَى إِلَى المُصَلَّى»

**"Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alikuwa anatoka siku ya Eid al-Fitr na Eid al-Adh'ha kwenda (kuswali) kwenye kiwanja cha wazi"**[6]**.**

Amesema Ibn Hajar -Allaah amrehemu-:

"وَفِيهِ الْخُرُوجُ إِلَى الْمُصَلَّى فِي الْعِيدِ وَأَنَّ صَلَاتَهَا فِي الْمَسْجِدِ لَا تَكُونُ إِلَّا عَنْ ضَرُورَةٍ"

**"Katika hadithi hii kuna faida ya kwamba (sunnah) ni kutoka kwenda kuswali Eid kiwanjani, na wala haitaswaliwa msikitini ila kwa dharura".**

Na Sehemu nyingine amesema:

"وَاسْتُدِلَّ بِهِ عَلَى اسْتِحْبَابِ الْخُرُوجِ إِلَى الصَّحْرَاءِ لِصَلَاةِ الْعِيدِ وَأَنَّ ذَلِكَ أَفْضَلُ مِنْ صَلَاتِهَا فِي الْمَسْجِدِ لِمُوَاظَبَةِ النَّبِيِّ صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ عَلَى ذَلِكَ مَعَ فَضْلِ مَسْجِدِهِ وَقَالَ الشَّافِعِيُّ فِي الْأُمِّ بَلَغَنَا أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ كَانَ يَخْرُجُ فِي الْعِيدَيْنِ إِلَى الْمُصَلَّى بِالْمَدِينَةِ وَكَذَا مَنْ بَعْدَهُ إِلَّا مِنْ عُذْرِ مَطَرٍ وَنَحْوِهِ وَكَذَلِكَ عَامَّةُ أَهْلِ الْبُلْدَانِ"

**"Pametolewa ushahidi kwa hadithi hii kwamba sunnah ni kutoka kwenda kuswali Eid majangwani, na hilo ndio bora zaidi kuliko kuswali msikitini, kwa sababu ya kudumisha kwake Mtume -Swala na Salamu zimshukie- sunnah hiyo, pamoja na fadhila za msikiti wake. Amesema Imam Shafi' katika Al-Ummu: imetufikia hadithi kwamba Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alikuwa anakwenda kuswali Eid mbili kiwanjani huko madina,**

---

[5]- Fat-hul baari (Jz. 2, Uk. 447).
[6]- Bukhari (956) na Muslim (890).

**pia walifanya hivyo waliokuja baada yake, isipokuwa ukipatakana udhuru wa mvua n.k, na wanafanya hivyo watu wa miji yote"[7].**

4. **Sunnah ni kwenda kiwanjani kwa kutembea kwa miguu:**

Kutoka kwa Ally -Allaah amridhie- amesema: **"Sunnah ni kuwa utoke kwenda kwenyе kuswali Eid hali ya kuwa unatembea"[8].**

5. **Sunna ni kubadilisha njia wakati wa kurudi:**

Kutoka kwa Abu Huraira -Allaah amridhie- amesema: **"Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alikuja kwenye swala ya Eid akiwa anatembea (bila kipando), na anarudi kwa njia nyingine tafauti n njia aliyoendea"[9].**

Amesema Imam Shafi' -Allaah amrehemu-:

"فَأُحِبُّ ذَلِكَ لِلْإِمَامِ، وَالْعَامَّةِ"

**"Napenda kufanya hivyo kwa imam na watu wote"[10].**

6. **Wakati wa swala ya Eid:**

Wakati wa swala ya Eid unaingia baada ya kupanda jua kiasi cha urefu wa upinde tangu kuchomoza kwake, Abdullaahi Bin Busri -Allaah amridhie- mara moja alienda kwenye Eid al-Fitri au Eid al-Ad'ha akachukia kuchelewa kwa imam akasema: **"Hakika tulikuwa sisi wakati huu tumeshamaliza swala, nao ni wakati wa Tasbiih (mwanzo wa wakati wa swala ya dhuha"[11].**

---

Baadhi ya maulamaa wamekadiria mwanzo wa swala ya dhuha ni kiasi cha dakika 13 tangu kuchomoza kwa jua, na Eid al-Adha (Eid ya kuchinja) ni vizuri kufanya haraka.

---

7- Fat-h al-Baari (Jz. 2, Uk. 450).

8- Sunan Tirmidh (530).

9- Sunan Ibn Maajah (1300).

10- Al-Ummu (Jz. 1, Uk. 267).

11- Abu Daud (1135).

## 7. Namna ya kuswali swala ya Eid:

Swala ya Eid ni rakaa mbili, utapiga Takbira saba katika rakaa ya kwanza baada ya Takbira ya kuhirimia, na utasoma dua ya kufungulia swala, na katika rakaa ya pili utasomaTakbira tano tafauti na takbira ya kunyanyuka kutoka kwenye sijda ya pili ya rakaa ya kwanza.

Kutoka kwa Aisha -Allaah amridhie- amesema: **"Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alipiga takbira saba (katika rakaa ya kwanza) na takbira tano (rakaa ya pili) katika swala ya Eid al-Fitr na Eid al-Adh'ha"[12].**

## 8. Sunna katika swala ya Eid ni kusoma sura zifuatazo:

Katika rakaa ya kwanza utasoma Surat al-Faatiha na Surat Al-A'laa, na katika rakaa ya pili utasoma Surat al-Ghaashiyah, kwa hadithi ya Nu'maan Bin Bashir -Allaah amridhie-: **"Mtume -Swala na Salamu zimshukie- alikuwa anasoma (rakaa ya kwanza) Sabbihisma na (rakaa ya pili) Hal ataaka, katika swala ya Eid mbili na siku ya Ijumaa, na endapo zimekusanyika Eid na Ijumaa katika siku moja, anazisoma sura hizo katika swala mbili zote"[13].** Na katika riwaya nyingine Omar alimuuliza Abu Waaqid Al-Laythiy Allaah awaridhie- kuhusu kisomo cha Mtume -Swala na Salamu zimshukie- katika swala za Eid mbili akasema:

«كَانَ يَقْرَأُ فِيهِمَا بِ ق وَالْقُرْآنِ الْمَجِيدِ، وَ اقْتَرَبَتِ السَّاعَةُ وَانْشَقَّ الْقَمَرُ»

**"Alikuwa anasoma katika rakaa mbili hizo, surat Qaaf na surat Al Qamar"[14].**

---

12- Sunan Ibn Maajah (1280).

13- Muslim (878).

14- Muslim (891).

## 9. Takbira za Eid na wakati wake:

Ni sunah kuleta Takbira katika sikukuu za Eid mbili, na imekokotezwa zaidi katika Eid al-Fitr kwa kauli yake Allaah:

﴿وَلِتُكْمِلُوا۟ ٱلْعِدَّةَ وَلِتُكَبِّرُوا۟ ٱللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَىٰكُمْ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ﴾

**"Na timizeni hiyo hesabu na mumtukuze Allaah (kwa kusoma takbira) kwa kuwa amekuongoeni, na ili mpate kumshukuru"**[15].

Imepokewa kutoka kwa baadhi ya Maswahaba kwamba, wao walikuwa wanaleta Takbira wakati wa kuelekea kwao viwanjani, na mwisho wake katika Eid al-Fitr pale atakafika imam kwa ajili ya swala. Ama Eidi al-Adh'ha, amesema Ibn Hajar -Allaah amrehemu-: **"Kauli sahihi iliyopokewa kutoka kwa Maswahaba ni kauli ya Ally na Ibn Masoud -Allaah awaridhie-: Kwamba (takbira) zinaanza asubuhi ya siku ya Arafa mpaka wakati wa alasiri siku ya mwisho ya kukaa Mina (tarehe 13 dhul Hijjah)"**[16].

## 10. Matamko ya Takbira:

Ama matamko ya Takbira yaliyo pokewa kutoka kwa Maswahaba ni:

الله أكبَرُ الله أكبَرُ الله أكبَرُ كبِيْرًا

**"Allaahu Akbar, Allaahu Akbar, Allaahu Akbar Kabiira"**[17].

الله أكبَرُ الله أكبَرُ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ ، اللَّهُ أَكْبَرُ وَلِلَّهِ الحَمْدُ

**"Allaahu Akbar Allaahu Akbar Laa ilaaha illaLlaahu wallaahu akbar, Allaahu Akbar walillaahil hamdu"**[18].

---

15- Al-Baqara/185
16- Fat-hul baari (Jz. 2, Uk. 462).
17- Al-Muswannaf (Jz. 2, Uk. 168).
18- As sharhul mumti' (Jz. 5, Uk. 227).

## Tanbih:

- Mwisho wa kuswali Eid ni baada ya kupondoka jua, kwa sababu hapoutakuwa umeingia wakati wa adhuhuri.
- Endapo mtu hakujua kwamba hiyo ni siku ya Eid isipokuwa baada ya kumaliza wakati wake, ataswali siku inayofuata kama alivyoswali imam, na kauli wengi katika maulamaa ni kwamba ataswali bila ya khutba hata kama wataswali kwa jamaa.
- Hakuna katika kiwanja cha Eid swala yoyote isiyo kuwa swalaya Eid, si kabla wala baada yake. Na endapo watu wameswali msikitini kwa dharura ya mvua n.k, basi ataswali mtu rakaa mbili za Tahiyyatul masjid.
- Wanawake ni haramu kujipaka manukato wakati wa kutoka nje ya nyumba zao, na vilevile ni lazima kuvaa nguo zenye kusitiri mwili mzima.
- Hakuna dua maalumu baina ya takbira moja na nyingine ndani ya swala.
- Haijathibiti kuleta Takbira katika viwanja vya Eid au misikitini kwa sauti ya pamoja, bali kila mtu atasome binafsi.
- Takbira za katika swala ya Eid ni sunnah, endapo mtu amesahau kusoma, hatoleta sijda ya kusahau.
- Haifai kwa maamuma kunyanyua sauti kwa Takbira au dhikri yoyote, sawa katika za faradhi au sunna.
- Haijathibiti katika uwanja wa Eid kuhutubu kwa mimbari.

- Khutba ya Eid ni moja tu na wala haifunguliwi kwa Takbira, sunnah ni kuanza kwa kumhimidi Allaah.
- Kusikiliza khutba ni sunna wala si wajibu, isipokuwa ni vizuri muislamu kubaki kwa ajili ya kupata faida.
- Haijathibiti kuhusisha siku ya Eid na kuzuru makaburi hiyo ni bidaa, mtu anaruhusiwa kuzuru siku yoyote, wala si kuhusisha ibada hiyo na siku ya Eid.
- Haijathibiti hadithi ya kutaja fadhila za kuswali usiku wa kuamkia Eid.
- Miongoni mwa makosa ni kauli ya baadhi ya maimamu: **'Mwenye kumuasi Allaah siku ya Eid ni sawa na kumuasi Allaah siku ya kiama"!!.** Maneno haya amezuliwa Mtume.

Wabillaahi Ttaufiq

**Imekamilika usiku wa**

**1/shawwaal/1447h – 20/03/2026m**